

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA BAJETI**

**TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI JUU YA MAPENDEKEZO YA  
MPANGO WA TAIFA UNAOKUSUDIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI  
PAMOJA NA MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA  
SERIKALI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17.**

OFISI YA BUNGE  
S.L.P 941  
**DODOMA**

**1 Februari, 2016.**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 naomba kuchukua fursa ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17 na mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 yanatoa mwanga wa jinsi bajeti na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 utakavyokuwa katika kuimarisha uchumi wa viwanda na kupunguza umasikini. Kwa upande wa mwelekeo wa mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vya kuendeleza viwanda ambavyo vitaimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kupaa (*Flagship project*) na maeneo yatayolenga kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Aidha, mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vitakavyotekelezwa na Serikali.

## **2.0 MAPITIO YA HALI YA UCHUMI JUMLA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015**

### **2.1 Ukuaji wa uchumi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimatafa (2015) inaonesha kuwa uchumi wa nchi zinazoibukia na zinazoendeleoa unatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2015 na asilimia 4.5 kwa mwaka 2016. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa asilimia 6.9 kwa mwaka 2015 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016. Hata hivyo hali hii ya ukuaji wa uchumi hapa nchini bado haijaweza kupunguza umasikini wa kipato kwa Wananchi hasa wa vijijini.

### **2.2 Pato la Taifa na Pato la Kila mtu**

**Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa Wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2014 na asilimia 7.1 mwaka 2015. Aidha, Pato la Taifa la Mwaka 2014 lilikuwa Shilingi trilioni 79.442 kwa bei ya mwaka husika na idadi ya watu ilikadiriwa kuwa watu milioni 46, hivyo pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,724,416 sawa na Dola za Kimarekani 1,038. Mwaka 2015 pato la Taifa lilikadiliwa kufikia shilingi trilioni 89.0 na pato la mwananchi kwa mwaka huo lilikadiliwa kuwa shilingi 1,828,022 sawa na dola za Kimarekani 1,043. Pamoja na jitihada za kuongeza Pato la Kila mwananchi bado tuko

mbali katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2025 ambayo imelenga kufika dola za Kimarekani 3,000.

### **2.3 Mfumuko wa Bei na Thamani ya Shilingi**

**Mheshimiwa Spika,** Mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 4.0 mwezi Januari 2015 hadi asilimia 6.4 mwezi Julai 2015 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 6.8 mwezi Disemba 2015. Kwa mujibu Taarifa ya Serikali inaonesha mfumuko wa bei umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongeza kwa bei ya vyakula. Hali hii inaonesha kwamba kuna tatizo la mgawanyo wa chakula nchini, kwani kwa kipindi cha mwaka 2014/15 nchi yetu ilikuwa na kiwango cha utoshelezi wa chakula kwa asilimia 125. Hivyo ni dhahiri kwamba kuna tatizo la mgawanyo wa chakula ambalo yawezekana linasababishwa na tatizo la miundombinu. Endapo kungekuwa na miundombinu thabiti ya utawanyaji wa chakula tatizo hili la mfumuko wa bei lingeweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi dhidi ya dola ilishuka kutoka shilingi 1,731.31 Januari 2015 hadi shilingi 2,149.1 Oktoba mwaka 2015. Pamoja na Sababu zilizotolewa na Serikali Kamati inaamini kwamba kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani kumechangiwa kwa kiasi na kuagiza bidhaa na huduma nyingi zaidi kutoka nje kuliko kiasi cha huduma na bidhaa tunazouza nje ya nchi. Mwaka 2015 thamani ya bidhaa tulizo uza nje ilikuwa dola za kimarekani milioni 9, 406.1 wakati thamani ya bidhaa na

huduma tulizoagiza kutoka nje zilifikia dola za kimarekani milioni 13,200.6 hivyo kutengeneza nakisi ya dola za kimarekani 4,002.0. Nakisi hii imeathiri Akiba ya fedha za kigeni ambayo mpaka kufikia Oktoba 2015 ilikuwa dola za kimarekani milioni 4,034.2 kiasi ambacho kinaweza kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi minne tu, hii ikiwa ni bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inaongeza kiwango cha Akiba ya fedha za Kigeni zinazoweza kugharamia mahitaji ya huduma na bidhaa kutoka nje kufikia walau miezi sita.

## **2.4 Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa limeongezeka kutoa dola za kimarekani milioni 18,643.8 mwezi Oktoba 2014 hadi kufikia dola za kimarekani milioni 19,221.4 mwezi Oktoba 2015. Deni hilo limeongezeka kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 5077.6. sawa na asilimia 3.0 kwa mwaka mmoja tu. Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe inatumia mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo tu. Aidha, Serikali ianze kuwa na utaratibu wa kushirikisha Bunge kabla ya kwenda kuchukua mikopo ili kupata maoni na mapendekezo.

## **2.5 Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa kipindi cha nusu mwaka 2015/16**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi trilioni 22.49. Kwa kipindi cha

Julai hadi Disemba 2015, Mapato yote ya Serikali yalikuwa jumla ya shilingi trilioni 10.23 hii ikiwa ni sawa na asilimia 88.8 ya makadirio ya nusu mwaka. Aidha, hadi kufikia Disemba 2015, Serikali imetoa mgao wa matumizi wenye thamani ya shilingi trilioni 10.31 sawa na asilimia 89 ya lengo la shilingi trilioni 11.53 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi trilioni 8.18 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.13 ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali haikuwasilisha utekelezaji wa nusu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/16 kwa vipaumbele vya kisekta. Hata hivyo mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/15 yameanishwa vizuri kwenye taarifa yake.

### **3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2016/17**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 na kutoa maoni na ushauri ufuatao:

#### **3.1 Ujumuishwaji wa vipaumbele vilivyopita**

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 hauna budi kuoanisha vipaumbele vilivyoshindwa

kutekelezwa ipasavyo katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2015/16 pamoja na kulinganisha yale yatakayokuwemo kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2016/17-2020/21. Lengo ni kuona na kujiuliza tumetoka wapi, tumefika wapi, tufanye nini ili Mpango unaokusudiwa utuelekeze kutekeleza malengo ya Dira 2025. Aidha, Mpango huo pamoja na **MKUKUTA II** ujikite katika kutoa majibu ya changamoto zilizopo katika kuondoa umaskini wa kipato. Kwa kufanya hivi tutahakikisha kuwa dhana ya ***kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa'*** inafungamana na dhana mpya ***'kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu'***.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Bunge kuangalia Mapendekezo ya Mpango huu katika sura ya Kitaifa na kutathmini mahitaji ya rasilimali inayohitajika katika kutekeleza mpango huu. Bunge lisimamie uzingatiaji wa vipaumbele tutakavyokubaliana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17-2020/21) hapo baadae viguse maeneo machache ambayo yataibua fursa za kiuchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini kupitia maendeleo ya viwanda. Aidha, ni vema sheria ya bajeti ikatekelezwa kikamilifu katika usimamizi mipango ya muda mfupi na mrefu.

### **3.2 Ugharamiaji wa miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanisha vyanzo mbalimbali vya kugharamia mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/17 ambavyo kwa

jumla vitatoa shilingi bilioni 6,182.2. Changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini ni mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Tathmini inaonesha katika mpango uliopita, pamoja na kuwa Serikali iliainisha vyanzo vya fedha katika kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kitaifa ya kimkakati, bado fedha hizo hazikupatikana kwa wakati uliopangwa au kutofika kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika. Kamati inashauri kuwa Serikali ijipange vema kuhakikisha inasimamia ipasavyo mapato ya ndani, mikopo na fedha za mifuko maalum (ringfenced) pamoja na sekta binafsi ili kuhakikisha inapata kiasi hicho cha fedha za kugharamia mpango husika. Aidha, Kamati inaona kuwa ni vema sasa Serikali ikaanza kuona namna ya kupata mapato kutoka katika sekta ya gesi kupitia Sera ya uanzishwaji wa Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi (Oil and Gas Fund) ambao utatumika kugharamia miradi ya maendeleo.

### **3.3 Utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Kielelezo (*Flagship Projects*)**

**Mheshimiwa Spika**, kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka miradi mikubwa ya kielelezo kama kipaumbele kikuu kimojawapo katika mpango unaotegemewa kutekelezwa. Kamati inaona kwamba, kama Serikali itafanikiwa kutekeleza miradi hii hasa ile ya maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) Bagamoyo, Mtwara, Kigoma, kituo cha biashara na huduma Kurasini (*Tanzania logistic hub*), mji mpya wa kilimo Mkulazi (Morogoro), ujenzi wa kiwanda cha chuma Liganga na ujenzi wa Reli ya kati; basi Serikali itakuwa imefanikiwa kwa kiasi



kikubwa kukuza uchumi wake kupitia upatikanaji wa ajira kwa wananchi, kuboresha miundombinu ya usafiri, pamoja na kuboresha shughuli za kilimo na viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, ipo haja ya kuona kuwa mpango huu unajielekeza katika kutoa matokeo chanya kwenye maeneo maalum ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje (EPZ/SEZ). Serikali iendeele kuhamasisha uwekezaji, ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya EPZ/SEZ na kutoa fidia kwa wakati ili kuruhusu utekelezaji wa miradi husika kwa wakati. Miradi hii ya EPZ/SEZ iliyopo na ile ambayo tunategemea itakamilika itakuwa ni mwanzo wa msingi mzuri wa mwendelezo wa ujenzi wa viwanda na hivyo kupiga hatua kwa upande wa ajira, soko la malighafi nchini, kuvutia wawekezaji na biashara na hivyo kuiingizia mapato ya kigeni na hatimaye kukuza uchumi wetu na kuelekea hadhi ya Nchi ya Kipato cha Kati. Aidha, Serikali iweke mazingira wezeshi ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kupitia sheria ya manunuzi ili kutowakatisha tamaa wawekezaji muhimu.

### **3.4 Usimamizi, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia kuwa Mapendekezo ya Mpango yawe ni dira ya kuagiza na kujenga nidhamu kwa vyombo vikuu vya kupanga, kufuatilia, kutathmini na kutekeleza Mipango ya Nchi. Mantiki ya maelezo yaliyotolewa ni kusisitiza kuwa Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2016/17 pamoja na kuelezea

misingi na shabaha na utayarishaji ni lazima vile vile uoneshe Mpango unaotarajiwa kujibu changamoto na vikwazo vya kinfumo (*structural rigidities*) vilivyojitokeza katika kuendesha na kusimamia Uchumi katika Mpango uliopita wa Mwaka 2015/16. Mapendekezo yasisitize na kuonesha suala la muda wa utekelezaji wa mradi (*timeline*), gharama ya mradi (*costs*) na uharaka (*urgency*) wa kupanga Mipango kwa Upande wa Serikali. Aidha, Mapendekezo haya ni vyema, pamoja na kujenga nidhamu, yasisitize umakini (*seriousness*) baina ya Wawekezaji, Watekelezaji na Watendaji katika ngazi zote za Serikali na sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeona bado kuna changamoto katika kuuelewa mipango, taratibu za usimamizi na ushirikiano wa vyombo vinavyosimamia Mipango ya Maendeleo kwenye ngazi mbalimbali za utawala na hivyo kusababisha kurudia mapungufu na makosa yanayojitokeza awali kwenye mipango husika. Aidha, baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikiandaa programu za kisekta ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa; ikiwa pamoja na kutumia fedha nje ya bajeti. Mapendekezo ya Mpango wa 2016/17 hayana budi kurekebisha mapungufu haya ili kutimiza malengo tuliyo jiwekea kwenye mipango husika. Aidha, ni vema Serikali ikawa na utaratibu maalumu wa kupanga bajeti ya utekelezaji wa vipaumbele vikubwa (uchaguzi mkuu, vitambulisho vya taifa na katiba mpya) kwa awamu.

### 3.5 Uendelezaji wa Sekta ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika**, mwelekeo wa utekelezaji wa mpango pili wa maendeleo wa Taifa ni kuweka mazingira wezeshi na endelevu kwa ajili ya ukuaji wa viwanda kupitia sera na mikakati madhubuti ikiwa pamoja na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi. Kamati inaelewa kuwa sekta ya viwanda haiwezi kupiga hatua bila kuweka mazingira mazuri ya kuiendeleza. Kamati inashauri serikali kuhakikisha inafanyia kazi eneo la kupunguza gharama za uzalishaji, kwa mfano upatikanaji wa umeme wa kutosha, kupunguza urasimu pamoja na kusimamia vizuri sera za kodi na fedha (*fiscal and monetary policies*) ili ziweze kuleta matokeo tarajiwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa pamoja na Mipango mingine tuliyopanga kwenye sekta ya viwanda, ni muhimu mpango huu wa mwaka mmoja ukajielekeza katika kuhusisha mikakati mbalimbali ya kuendeleza sekta za viwanda vidogo vidogo, kuongeza thamani ya bidhaa zetu pamoja na kuongeza mauzo nje. Aidha ni muhimu mpango huu ukajielekeza pia katika kufikiria namna mchakato wa ujenzi wa viwanda vipya, kufufua na kukarabati viwanda ambavyo havifanyi vizuri na kufufua vile vilivyokufa. Aidha Mpango huu uhusishe Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Sekta ya Viwanda (*Integrated Industrial Development Strategy and Master Plan*) ambao unaibua mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha kuendeleza Viwanda na kukuza mauzo nje (*Water Front Industrial and Export Frontiers*) ikiwa pamoja na kulenga kufanya usindikaji wa

mwanzo (*primary processing*) kwenye maeneo ya mbalimbali ya mikoani na mwambao wa pwani.

### **3.6 Maeneo wezeshi ya maendeleo ya Viwanda (Klimo, Ardhi, Mifugo na Uvuvi)**

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu unaonesha kuwa nchi nyingi duniani zimepiga hatua za uchumi wa viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa ya kukuza uchumi wetu (Pato la Taifa) na ushindani wa kikanda na kimataifa kupitia sekta husika.

### **3.7 Mapitio ya Sheria za Ubia na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaishauri Serikali kuhaulisha sheria zote zinazohusiana na masuala ya Uwekezaji pamoja na ubia nchini. Mfano *Tanzania Investment Act 1997, Export Processing Zone Act 2006, Mining Act 2010, Public Private Partnership Act, 2010 na Public Procurement Act, 2011*. Kuhaulishwa kwa sheria hizi kutahamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika utekelezaji wa Mpango huu kwa sababu taratibu za uwekezaji na ubia katika Sekta mbalimbali zitakuwa chini ya mwavuli mmoja. Aidha, kupitia Sheria hizi Sekta ya Umma kushirikiana na Sekta Binafsi zitapata fursa

za kujenga, kuendesha na kuwekeza katika miradi muhimu ambayo itasaidia kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na kuwawezesha wananchi kupata ajira na kuongeza kipato kupitia miradi hiyo ya uwekezaji na ubia.

Aidha, Kamati ya bajeti inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa hapo awali kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya kuaandaa mfuko wa uwekezaji utakaowezeshwa kutoka katika gawiwo na mapato mbalimbali ili kunusuru hisa za Serikali na pia Serikali kuendelea katika kuwekeza katika sekta zingine ambazo itaona zinahitaji ushiriki wake kwa kupitia sheria ya ubia (PPP).

### **3.8 Mapendekezo ya jumla**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapendekezo tuliyatoa hapo juu, kwa ujumla Serikali ijielekeze katika kutoa majibu ya haraka kwenye kutatua changamoto za uhaba wa umeme na maji, ushindani usio wa haki, miundombinu duni, uhaba wa mitaji na fedha, upatikanaji wa masoko, ukosefu wa wataalamu na teknolojia duni, utatuuji wa sheria zinazokinzana katika uwekezaji, ufinyu wa bajeti na rasilimali watu na upunguzaji wa madeni makubwa ya Serikali.

### **3.0 MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17.**

**Mheshimiwa Spika,** Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi trilioni 22.99 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17. Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa Shilingi trilioni 15.80. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni Shilingi trilioni 14.10, mapato yasiyo ya kodi ni Shilingi trilioni 1.11 na Shilingi bilioni 584.4 ni mapato ya Halmashauri. Serikali inategemea kupata kiasi cha Shilingi trilioni 2.10 ikiwa ni misaada na mikopo kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17. Vile vile, Serikali inatarajia kukopa kiasi cha shilingi trilioni 1.78 kama mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara ili kupunguza nakisi ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali katika mwaka 2016/17 yanategemewa kuwa Shilingi trilioni 22.99 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 16.80 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha Shilingi trilioni 6.65 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali. Aidha matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi trilioni 6.18 ambapo kiasi cha Shilingi trilioni 4.81 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 1.37 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia mwongozo wa Bajeti kwa mwaka 2016/17 na kwa kiasi kikubwa inaipongeza Serikali katika

Maboresho ya Mfumo wa ukusanyaji wa mapato, Shabaha za uchumi jumla na misingi iliyowekwa kwa ajili ya Bajeti. Hata, hivyo Kamati ina ushauri ufuatao katika Mwongozo huo wa Bajeti:-

- 4.1 Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia mfumo wa ukadiriaji wa majengo kwa mkupuo (mass valuation) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote katika ukusanyaji wa kodi za majengo. Aidha, Majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa viwango vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi.** Katika mfumo wa ukadiriaji wa majengo kwa mkupuo (mass valuation); kamati inashauri kwamba Serikali iangalie hali ya uchumi ya eneo husika, thamani ya ardhi kwa maeneo husika na thamani ya nyumba yenyewe.
- 4.2 Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuboresha mazingira ya urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi.** Katika kufanikisha hili Kamati inaona kwamba umefika wakati muafaka kwa Serikali kutekeleza Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (**MKURABITA**) na mpango wa kuboresha mazingira ya biashara Tanzania (**Road Map for Improving Bussnes Enviroment in Tanzania**). Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikiria Kupima na kuanisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati miliki.
- 4.3 Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya;** Kamati inaipongeza Serikali kwa

hatua hii, hata hivyo Kamati inashauri ni vema tahadhari ikachukuliwa ili kuepusha migogoro ya kimkataba na wawekezaji katika Sekta mbalimbali.

**4.4 Mheshimiwa Spika, *Serikali inakusudia kufuta utaratibu wa 'retention' uliokuwa ukitumika awali na badala yake imeamua mapato yote yatakusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa watatakiwa kuwasilisha mapato yote yatakayokusanywa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti zitakazoidhinishwa katika mafungu hayo.*** Kamati inaunga

mkono kusudio hili, hata hivyo kamati inaishauri Serikali ikapitia sheria zilizoruhusu utaratibu wa '*retention*' wa kila taasisi ili kuepuka mgongano wa kisheria unaoweza kudhoofisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya taasisi husika.

**4.5 Mheshimiwa Spika, *Serikali imedhamiria kwamba Mashirika ya umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendeshe kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Mashirika hayo ni pamoja na TANESCO, TAZARA, TRL, ATCL, RAHCO, TEMESA, Wakala wa Vipimo (WMA), na Bodi ya Mazao Mchanganyiko.*** Moja ya sababu ya kutokufanikiwa kwa mashirika mengi ya umma ni madeni ambayo mashirika hayo yalikuwa yanaidai Serikali kutolipwa kwa wakati. Kamati inakubaliana



na uamuzi huu hata hivyo ni muhimu Serikali ikalipa madeni na ikawekeza vya kutosha na kuwekewa malengo utekelezaji wa majukumu katika mashirika haya ili yaweze kufanya kazi na kuzalisha faida.

- 4.6 Mheshimiwa Spika, *Serikali imeamua kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (courier), matangazo na usafiri.*** Kamati inaipongeza Serikali katika suala hili, hata hivyo Serikali iweke utaratibu wa kulipia huduma hizi kwa wakati ili kuepuka madeni mapya ya Serikali kwa taasisi husika kama ilivyo sasa. Aidha, ili lengo hili liweze kufanikiwa ni vema sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 ikafanyiwa marekebisho kurahisha suala hili. Aidha, ni sasa ni wakati muafaka wa kupata huduma muhimu ya mashirika ya umma kama TBC, TTCL, ATCL,TRL, TEMESA,TBA n.k
- 4.7 Mheshimiwa Spika, *Serikali kutenga kiasi cha asilimia 35 ya makusanyo yote ya Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo.*** Kamati inaona kuwa lengo hili ni muhimu likaonekana katika sura ya bajeti ijayo ili iendane na mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/17.
- 4.8 Mheshimiwa Spika,** Mwongozo uliowasilishwa na Serikali haujaweza kubainisha utaratibu wa madeni ya wazabauni na Wakandarasi ambao wanaidai. Kutokubainisha madeni hayo kwenye mwongozo wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17 hauleti picha

halisi ya utekelezaji wa bajeti itakayokuja hasa katika uhakika wa kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo. Kamati inaitaka Serikali kuweka wazi madeni ya wakandarasi na wazabuni kabla ya kuanza mwaka mpya wa fedha.

**4.9 Mheshimiwa Spika,** Kamati ingependa kupata ufafanuzi kuhusu kushuka kwa gharama ya mafuta mazito kwenye soko la dunia ukilinganisha na bei ya umeme unaozalishwa na mitambo inayotumia mafuta mazito hapa nchini. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya kamati haijafafanua vizuri kuhusu suala hili hasa ukizingatia kwamba umeme ni nishati muhimu katika kuharakisha maendeleo ya viwanda.

## **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2016/17 pamoja na mwongozo kwa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali

yaliyohusu mpango husika. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat S. Kandege, Mb - M/Kiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb
5. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
6. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
7. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
8. Mhe. Maria Ndila Kangonye, Mb
9. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
10. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Fletei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
15. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
16. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
17. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
18. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
19. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
20. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
21. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
22. Mhe. David Ernerst Silinde, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ni mpya na imefanya kazi kwa kujituma na kwa muda mfupi na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretariati ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Hawa A. Ghasia, Mb

**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

01 Februari, 2016